# HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU

OFISI YA MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IMALASEKO ,
S.L.P. 234,
**MEATU.**

**Kumb. Na.** ISS/ S. 2616/JI/VOL.I/14

11/12/2020

**Mob**. 0716442267

Jina la Mwanafunzi ..............................
..............................................................
ANWANI ...............................................
..............................................................

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IMALASEKO WILAYA YA MEATU MKOA WA SIMIYU.**

## 1.0. UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari IMALASEKO ipo umbali wa kilometa 52 Kusini mwa Mji Mkuu wa Wilaya ya Meatu.

Muhula wa kuanza unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **06/01/2021 Saa 1:30 Asubuhi** na mwisho wa kuripoti ni tarehe**20/01/2021. Baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Wazazi/Walezi wasiowaleta watoto wao kusajiliwa Shuleni.**

Tafadhali sana soma viambata vya barua hii na uzingatie maelekezo ili kutekeleza kuripoti mapema kwani tutaanza kufundisha tarehe 11/01/2021

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana

Wako,

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IMALASEKO
S.L.P. 234
MEATU.

.................................................
DEUSDETH J. SAFARI
**MKUU WA SHULE**

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1. Sare za shule

(a) **Wavulana** suruali mbili (2) na **tai** rangi ya **damu ya mzee** zenye malinda mawili **isiwe modo** na shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi.

(b) **Wasichana** sketi mbili (2) na **tai** rangi ya **damu ya mzee** zenye malinda, urefu wa sketi zenye **kufikia Jicho la Mguu [ANKLES]** na shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi

(c) Viatu vya shule ni vya ngozi, vyeusi vya kufunika, visigino vifupi na vyenye kamba kwa wote

(d) Soksi kwa wasichana ni nyeupe ndefu na kwa wavulana ni nyeusi ndefu za wastani

(e) Aje na nguo za michezo bukta, Tisheti ya damu ya mzee pamoja na raba

### 2.2. Vifaa vya masomo

- Daftari kubwa (counter books, Quire two au three) = **09**
- Daftari kubwa za kawaida **09** kwa ajili ya **majaribio ya kila wiki**
- Kalamu za kutosha na mkebe wa hesabu (Mathematical set)

**2.3.** Ni jukumu la mzazi, mlezi kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata **chakula** cha mchana shuleni

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
(h) Kutunza mali za umma
(i) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(j) Kufanya **Mazoezi , Majaribio na Mitihani** itakayotolewa na Walimu.

**Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule**

(a) Wizi
(b) Uasherati na Ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, milungi, kubeli n.k.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea, kuchokoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kumiliki/kuwa na **SIMU** Shuleni.

# BY: UTAWALA

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be completed by a medical Officer)

Student's full name: ……………………………………………………………………………………

Date of birth ……………………………………………………………………………………………..

A student has been tested for:-

a) Tuberculosis: …………………………………..…………………………………………

b) Blood count (red and white): ……………………………………………………………

c) Stool ……………………………………………………………………………………..

d) Urine ……………………………………………………………………………………

e) Syphilis …………………………………………………………………………………

f) Eye disorder ……………………………………………………………………………..

g) Ear disorder ……………………………………………………………………………...

h) Throat and chest ………………………………………………………………………

i) Spleen: …………………………………………………………………………………..

j) Pregnancy: ………………………………………………………………………………

k) Asthma: …………………………………………………………………………………

l) Allergic disorder: ………………………………………………………………………

**N.B** if yes/ positive please you advice us on how to help our student

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

**ANY ADDITIONAL INFORMATION** e.g physical defects, chronic or family disease etc

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

I certify that the above student is **fit / not fit** to pursue further studies.

Signature: ……………………………………

Designation: …………………………………..

Station: ………………………………………

Date: …………

Official stamp………….